Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims | Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Aya 215: Watoe Nini?

## Maana

**Wanakuuliza watoe nini?**

Msemo unaelekezwa kwa Mtume (s.a.w.w.).

**Sema: Kheri yoyote mtakayotoa ni kwa ajili ya wazazi na akraba na mayatima na masikini na mwananjia. Makusudio ya neno kheri hapa ni mali.**

Wazazi wawili ni baba, mama, babu na bibi, kwa sababu wao wanaingia katika jina la wazazi wawili. Ndugu ni akraba wa karibu wa mtoaji, yatima ni asiyekuwa na baba na mwana njia ni yule aliyeishiwa njiani na kushindwa kufika kwa watu wake na wala hana chakula.

Unaweza kuuliza kuwa dhahiri ya Aya inaonyesha kuwa watu waliuliza aina ya kitakachototolewa sio nani wa kumpa. Na jibu ni la matumizi sio la aina, sasa je, imekuwaje?

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya jawabu ni kumzindua muulizaji kwamba yeye anatakikana kuuliza nani wa kumpa, sio nini atoe. Razi amemnakili Qafal kwa jibu jingine; nalo nikuwa hata kama swali liko kwa tamko la Ma (nini) lakini kilichoulizwa ni nani wa kumpa sio cha kutoa, kwa sababu cha kutoa kinajulikana.

Sheikh Muhammad Abduh ameyatilia mkazo hayo kwa kauli yake: "wasomi wa fani ya mantiki ndio waliosema, swali la Ma linahusika na aina na jinsi..."

Lakini waarabu wanatumia kwa aina. Qur'an haiko katika mfumo wa Aristotle na mantiki yake, isipokuwa iko katika mfumo wa lugha ya Kiarabu ulio waziwazi. Jibu hili lina nguvu kuliko la kwanza ingawaje natija ni moja.

Swali la pili: “Je kuwapa waliotajwa katika Aya hii, ni wajibu au sunna? Jibu: Ni wajibu kwa wazazi kuwalisha watoto, na watoto kuwalisha wazazi ikiwa upande mmoja una uwezo na mwengine hauna uwezo wa kujilisha wenyewe. Kutoa huku hakuhisabiwi kuwa ni zaka. Ama mayatima na wasafiri,

inajuzu kuwapa kutokana na zaka ya wajibu; kama vile ambavyo inajuzu kuwapa wote sadaka ya sunna.

Na sadaka ya suna hupewa kila mwenye kuhitajia, awe Mwislamu au si Mwislamu, kwa sababu kuna malipo katika kumnywesha kila mwenye ini la joto (kiu); kama ilivyoelezwa katika Hadith.

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ ۖ
وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ {216}

Mmeandikiw

a

kupigana

(vita

)

nal

o

n

i

(jambo

)

la

kuchukiza kwenu. Na huenda mkachukia

kitu nacho ni

kher

i

kwenu

,

n

a

huenda

mkapend

a

kit

u

nach

o

ni

shari

kwenu. Na

Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ۖ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ۖ وَصَدٌّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ
وَكُفْرٌ بِهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ
الْقَتْلِ ۗ وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَنْ دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا ۚ وَمَنْ يَرْتَدِدْ
مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۖ
وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ {217}

Wanakuuliza juu ya

kupi

gan

a

(vita

)

katik

a

mwezi

mtakatifu. Sema: Kupigana vita katika (miezi) hiyo ni

(dhambi

)

kubwa

.

Na kuzuili

a

wat

u

n

a

nji

a

ya Mwenyez

i

Mung

u

na

kumkufuru na (kuwazuilia) Msikiti

Mtakatifu

na

kuwa

to

a

hum

o

wenyew

e

ni kukubw

a

zaid

i

mbel

e

ya

Mwenyezi

Mungu. Na fitina ni kubwa zaidi kuliko kuua. Wala hawataacha

kupigana nanyi mpaka wawatoe katika dini

yenu,

kama waki

weza

.

N

a

yeyot

e

katika nyiny

i

atakayertadi

,

kisha

akafa hali ya kuwa kafiri, basi hao zimepomoka amali zao

duniani

na akhera.

Na hao

ndio watu

wa motoni, humo

watakaa

milele.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ
اللَّهِ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ {218}

Hakika wale

walioamini

na

wal

e

walioham

a

na

wakafanya jihadi katika njia

y

a

Mwenyez

i

Mungu

,

hao

ndio wenye kutaraji

r

ehema

y

a

Mwenyez

i

Mung

u

na Mwenyez

i

Mung

u

ni

Mwenye

kughufiria,

Mwenye ku

r

ehemu.

**Source URL:** https://www.al-islam.org/sw/al-kashif-juzuu-ya-pili/aya-215-watoe-nini